wako bibi

Kwa nini wadada hawapendi kuwa madereva wa taxi ?

jijini, hata katika miji mikuu, ni haba kuta akina dada ama mama fulani akiongoza ri ya taxi. Akina dada Bujiriri Mwangaza utolea katika mistari ifuatayo jambo linalo-sukuma wabibi waepuke kazi hiyo.

ufuatana na mipango wakoloni,mtoto mwa-ke hakuwa na ruhusa kujielimisha haizuru tika masomo gani ao tumika kazi yoyote. kati ule kulionekana tafauti kubwa kati wavulana na wana-ke.

limu ya wabinti ili-wa zikiwaelekea tu naume.

sha nchi yetu kuji-tia uhuru,mabadiliko ngi yalionekana.

Mtoto binti ambaye alikuwa akibaki nyuma, alianza naye kusonga mbele kama vile mwenzie mwanaume. Alipewa naye uwezo wa kusoma kama mme na kutumika kazi zote.

Katiba (constitution) ya nchi yetu nayo imempatia uwezo na madaraka mengi.

Tangu hapo,twaona sasa wengi wao waanza kufanya kazi kama ile ya kalani. Ni wachache tu ndio wamejitupa katika uwi-to wa kidereva. Mfano tutakaotaja hapa ni ule wa yule mama ambaye alikuwa hapo majuzi na kazi za kuwachukua katika gari wafanya kazi wa shirika linalohusika na utengenezaji wa mabarabara (Office des routes).

Wengi husema kuwa upuuzi huo wa kazi ya kidereva wa taxi kwa akina dada kwatokana na demba. Wadada hao husema eti: "siwezi kuwa dereva wa taxi ao kutumikia shirika fulani. Kazi hiyo hainistahili, hainienei."

Tuonavyo sisi,wadada hao wamesahau fumbo la Wafaransa linalosema:" hakuna kazi mbaya ila watu wanaoitumika ndio hawajui kutumiya akili yao kama inavyostahili". Wamama wengi watamani wawe tu wanaongoza gari za mabwana wao na kujipiga kifuani eti wanavuma katika "succès". Lakini ukiwauliza kwa nini hawawezi kutumika kazi ya kidereva kusudi ya kufyonza feza za matajiri,watakujibu kuwa dereva ni kama vile mtumwa !

Enyi akina dada,kazi zote zina mafaa. Haifai kufuatana na manongonezo mabaya ya wavivu na wapenda raha ambao pia ni wazembe.

Muwe hakika kama hakuna kazi mbaya. Kila kazi ina matunda yake,yafaa tu mwenyeji aifanye kwa zamiri na uaminifu.

Tunafungua hapa karasa zetu kwa yeyote anayetamani kutoa maoni yake juu ya jambo hilo.

Bujiriri Mwangaza.

BUMBUAZI !

MALIMA AMEKWEPA

Ebu wakaaji wa mji wa Bukavu,msipate mshangao. Akida Malima aliyemuua mwananchi Makombo amekwisha kujimwanga porini.
Kisha kuhukumiwa kifo,jamaa huyo alitupwa gerezani ambako alibaki muda wa miezi michache akingojea hukumu yake ya mwisho.
Ni hivi,mnamo usiku wa tarehe 24 kuamkia 25 desemba 1984 jambazi Malima alifyatuka na kujielekeza nafasi isiyojulikana akimpeleka pia mchungaji wake.
Kumbe kituliro hakina tena mipaka ?

JUA

Gazeti la Kivu

BUKAVU

Ni kipindupindu ao kuhara tu ?

Siku hizi,wakaaji wa mji wa Bukavu na wale wa kando kando waendelea kunongoneza kuhusu magonjwa makali yanayowatetemesha. Ni pamoja na kuhara bila kiasi, kupatwa na kisonono, kifua kikuu, malaria.
Bila kusahau kipindupindu (choléra).
Magonjwa hayo ya kuambukia yatokana hasa na upuuzi wa kanuni za afya. Hapo majuzi, kiongozi wa mtaa wa Kadutu,mwananchi Kalumuna Heshima alimfikia mganga mkuu wa mji wa Bukavu,mwananchi Mutombo ili ampashe namna gani wakaaji wa Bukavu kwa jumla na wale wa mkoa wa Nyamugo kwa upekee wanashambuliwa na magonjwa ya kuhara. Habari hiyo,ilimshtua mganga Mutombo mpaka akachukua hatua ya kujielekeza huko Nyamugo kwa kujionea mwenyewe visa vya ugonjwa huo.
Kisha Kadutu,ugonjwa huo umekwisha kupiga hodi katika mitaa ya Ibanda (Mulengeza,Nguba) na Bagira ambako wakaaji wanaoshambuliwa wafariki kama vile nzige. Hapo hawali,mganga Mutombo alieleza kuwa Wakaaji wa Nyamugo walishikwa na ugonjwa wa kuhara bila kiasi kwani watumia maji inayotiririka katika mfereji unaounga "soko la bwaki" na hoteli Sisi kwa Sisi ya "Muganda Lumumba". Maji hayo yatumiwa kwa kufua nguo,kutayarisha chakula,kunawa mwili ao kusafisha vifaa vya jikoni.
Wakati tulipokuwa mitamboni,taarifa rasmi ya mganga ilieleza kuwa watu wengi wamekwisha kufariki kufuatana na visa vya ugonjwa huo.

Wasomaji wetu watakumbuka kuwa hapo hawali mganga alikuwa akiwaza kuwa ni ugonjwa wa kuhara tu. Lakini,kisha uchunguzi,katika vyumba vya dawa huko "Fomulac-Katana",ilionekana wazi kuwa huo ni ugonjwa wa kipindupindu ambao wajulikana sana kwa jina la "choléra".

Ni hivi,waganga waomba kwa kila yeyote anayetambua mtu anayeonekana na viini vya "choléra" ampeleke mbio hospitalini ambako atapewa matibabu inayoaminika.
Ila,haifai kusahau kanuni za afya: kutokosha maji mbele ya kuyanywa,kusafisha mikono kwa sabuni kisha kwenda chooni na mbele ya kula,kuepuka kula vyakula vibichi vinavyouzishwa ovyo ovyo njiani.

Kaboyi Habimana.

---

uzungumze

nicef yahimiza wazazi wachungue afya ya watoto wao

nanchi Lubunga, mwanafunzi kunako chuo cha upashaji wa habari huko Kinshasa(ISTI) aye aliye pia mwandishi wetu maalum, atoa machache kuhusu shirika linalohusika na ngo wa watoto duniani kwa kifupi UNICEF.

irika la Umoja wa aifa linalohusika na ngo wa watoto (UNI-F),limetangaza ya mba zaidi ya watoto ioni 1,2 wanafariki a mwaka kabla ya fikia umri wa miaka ano. Wengi kati ya oto hao hufariki okana na magonjwa ayo yanaweza tibiwa esi ao kuepukwa kwa isi.

na James Grant, rugenzi mtendaji ecteur exécutif) wa F alitangaza i kwenye mkutano nuko, Amman nchini ania,ya kama shirika litazidi kujikaza kurekebisha hali ya ha ya watoto dunia-Kwa maoni ya kio-i huyo, watoto i wanafariki sababu ujinga (kutofahamu; ance) wa wazazi

kuepuka balaa hiyo ,shirika la UNICEF araji kutumia njia mbali ili kuwa-isha wazazi mapa-yao mbele ya wadogo. Njia ni kama vile a,serikali, vya radio,televi-pamoja na magazeti pia ya kama nchini Colombia (Amerika ya kati),makanisa yalijitwika jukumu,kwa muda wa wiki nzima,mahubiri yote yakielekea tu mambo ya usafi. Na hiyo iliwasukuma wazazi wengi kuwapeleka watoto kwenye vyumba vya kuchanjiamo ndui.

Jambo la maana pia ni msaada wa serikali ao viongozi wa nchi. Serikali inatoa mali kwa kulipa wafanya kazi katika ofisi zinazohusika na afya ya binadamu (hygiène). Lakini jambo la kushangaza, ni kuona kama vyumba hivyo havishurulike sana na usafi wa wakaaji, mifereji, vyoo na kadhalika,waheshimiwa hao wanajifungia tu maofisini mwao,wakingoja sijue nini,pengine mwisho wa mwezi.

Vipindi vya kuelimisha ni msaada mkuu kwa upande huo. Mipango mbali mbali ya kuchanja ndui kusudi ya kuepuka magonjwa kama vile suluba, ndui,kupoa viungo, na mengine mengi ni jambo linalopashwa kutukuzwa sana.

Lubunga B. M'kobya

Kisha Marekani

Uingereza yatisha kujiondoa katika Unesco

Ikifuata mfano wa shirikisho la Amerika,serikali ya Uingereza imechukua hatua ya kujiondoa katika shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu Sayansi,Utamaduni na Maadibisho, kwa kifupi UNESCO.
Serikali ya Uingereza inayoongozwa na akina bibi Margaret Tatcher yatisha kuondoka katika Unesco mnamo mwaka 1986 ikiwa mashurti yake hayatakubaliwa na viongozi wa Unesco.
Uingereza inawashtaki viongozi wa Unesco kwa matumizi mabaya ya feza. Zaidi ya hayo, shirika hilo latia mkazo juu ya jambo l[illegible]
Ikiwa mabadiliko haya[illegible] kwenyi uongozi wa Unesco, Uingereza itajiendea lwake mnamo mwaka 1986 ikifuata mfano wa Marekani.

Kuondoka kwa nchi hizo mbili katika UNESCO ni mzigo mkubwa na mzito kwa shirika hilo la kimataifa. Kwani UNESCO yatumia feza za mchango (cotisation) kutoka nchi za- nachama. Marekani na Uingereza zitakapoondoka, feza za UNESCO zitapunguka sana. Kwa maana nchi hizo ni baina ya zile zinazotoa michango inayoaminika.

Kufuatana na maoni ya wachunguzi, inasemekana kuwa jambo hilo latokana na propaganda mbaya ya kutaka kumuangusha mkurungezi mtendaji wa UNESCO, bwana Amadou Mahtar M'bow, mzaliwa wa Sénégal. Nchi hizo tajiri hazifurahi kumuona mwenyekiti wa asili ya kiafrika kusimamia shirika kama vile Unesco.

Akijibu kwa maswali ya wapashaji wa habari wa redio na magazeti mbali mbali ya kiafrika,bwana M'bow alisema kuwa ataraji(angoja) kujiuzulu (démissionner) ingawa nchi hizo zaendelea kumsengenya.
Kulingana na ripoti iliyofanywa na kamati ya uchunguzi wa feza za Unesco,hakukuonekana makosa yoyote,aliongeza kusema bwana Amadou Mahtar M'bow.

Kaboyi Habimana na
Lubunga Bya'ombe.